

SWALI: Mwandishi wa kitabu cha Mithali alikuwa nani?

Sulemani mwana wa Daudi, anajitaja mwenyewe kama mwandishi, katika mwanzo kabisa wa kitabu hiki

Mithali 1:1 Mithali za Sulemani, mwana wa Daudi, mfalme wa Israeli.2 Kujua hekima na adabu; kutambua maneno ya ufahamu

Kitabu hichi kinakadiriwa kuandikwa miaka mia tisa (900) kabla ya Kristo. Ni kitabu kilichojaa maneno ya hekima na kanuni, maagizo ya rohoni, vilevile maonyo mbalimbali yanayohusiana na maisha ya kawaida, pamoja na maarifa na mafunzo yaliyo katika vitu vya asili.

Migawanyo yake:

Mithali 1-22:16, Iliandikwa na Sulemani mwenyewe.

Kuanzia Mithali **22:17-24:34**, zilizojulikana kama kitabu cha Tatu, huwenda ziliandikwa na wengine lakini zikakusanywa na Sulemani mwenyewe.

Lakini Kuanzia **Mithali 25-29**, biblia inatuambia ziliandikwa na Sulemani, lakini watu wa mfalme Hezekia ndio waliozirekodi.

Na **Mithali 30**, Ambacho hujulikana kama kitabu cha Tano. Kiliandikwa na Aguri bin Yake.

Lakini **Mithali 31** ambacho ni cha mwisho, kiliandikwa na mfalme Lemueli.

Japo wanazuoni wengine husema Aguri bin yake na Lemueli, yalikuwa ni majina mengine ya Sulemani.

Kwa vyovyote, kitabu hichi kwa sehemu kubwa kimeandikwa na Sulemani. Ndio maana hujulikana kama kitabu cha Sulemani. Lakini pia hatuna uhakika asilimia zote hekima zote ziliandikwa na yeye mwenyewe, kufuata na hao watu wawili wa mwisho wasiojulikana.

Kwa urefu wa chambuzi wa kitabu hichi fungua link hii >> [VITABU VYA BIBLIA: Sehemu ya 11 \(Mithali, Wimbo ulio bora, Mhubiri\)](#)

Hizi ni baadhi ya fafanuzi ya hekima tuzisomazo katika kitabu hicho

Maana ya Mithali 21:17 Mtu apendaye anasa atakuwa maskini;

Fahamu maana ya Mithali 10:5 Akusanyaye wakati wa hari ni mwana mwenye hekima;

Fahamu maana ya Mithali 25:13 Kama baridi ya theluji wakati wa mavuno;

Nini maana ya Mithali 5:15-18 anaposema Unywe maji ya birika lako mwenyewe?

Nini maana ya Mithali 21:1 Moyo wa mfalme huwa katika mkono wa Bwana;

Bwana akubariki.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge

na channel yetu kwa kupofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255789001312 au +255693036618

Bwana akubariki.

Mafundisho mengine:

Je! Sulemani alienda mbinguni?

NGUVU YA HEKIMA NA AKILI

TAFUTA HEKIMA, MAARIFA, UFAHAMU NA BUSARA.

Share on:

WhatsApp